ya kuchukua au kuchunguza sampuli toka kwa mtoto au mtu mwenye ulemavu wa akili, ila kibali hakitatakiwa kwa sampuli katika kesi za jinai.

- Kibali kitolewe na mhusika kwa ajili ya uchukuzi wa sampuli kwa utafiti.
- Iwe ni kosa kuchukua na kupeleka sampuli ya mtu kwa uchunguzi wa jenetiki bila ya kibali cha mtu huyo au mamlaka iliyoruhusiwa kisheria.
- Kianzishwe chombo cha kisheria cha kudhibiti maabara ambayo itashughulikia uchunguzi wa sampuli na pia kuishauri serikali kuhusu masuala ya sera ya vinasaba.
- Serikali ihakikishe kuwa watu wanapewa mafunzo ya kutosha katika kusimamia matumizi ya vinasaba.
- Vyombo vitakavyotumika kufanya uchunguzi wa vinasaba viwe ni vya kiwango na vya kutosha, na huduma zao zipatikane kwa urahisi.
- Kuelimisha umma kuhusu matumizi ya vinasaba.
- Sheria iainishe sifa za watu watakaokuwa na dhamana ya kupima sampuli hizo na wenye mamlaka ya kutoa majibu kwa walengwa na mtu anayepaswa kupewa majibu hayo.
- Sheria ya Ushahidi, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na Sheria ya Uchunguzi Rasmi wa Vifo zifanyiwe marekebisho ili kuruhusu matumizi ya teknolojia ya vinasaba.

## JE SHERIA YA KUSIMAMIA VINASABA IMEAINISHA NINI?

Sheria ya Usimamizi Vinasaba ya mwaka 2009 imebainisha mambo yafuatayo:-

- Kuanzishwa kwa ofisi ya msimamizi wa vinasaba katika ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ambayo inasimamia na kuendesha huduma hii ya matumizi ya vinasaba kulingana na masharti ya sheria husika.
- Utaratibu mzima wa uteuzi wa maafisa sampuli ambao wanahusika kuchukua, kuandikisha na kusafirisha sampuli za vinasaba vya binadamu kulingana na utaratibu uliowekwa kisheria.
- Kuanzishwa Maabara ya vinasaba vya binadamu ambayo itakuwa chini ya Wakala wa Maabara ya

*Tunahusisha yaliyopita, Tunatengeneza y a sasa na Kupanga ya baadae,*

Mkemia Mkuu wa Serikali.

- Utaratibu wa mtu binafsi kupata kibali au leseni ya kuanzisha maabara ya vinasaba.
- Utaratibu wa wahusika kuomba kufanyiwa uchunguzi wa sampuli za vinasaba ambao ni hawa wafuatao; Mahakama, Afisa Polisi mwenye ngazi ya Inspekta au juu yake, Wauguzi, Wakili, Taasisi ya Utafiti, Kamishna wa Wilaya wakati wa maafa makubwa na Afisa Maendeleo ya Jamii.
- Makosa mbalimbali yanayohusiana na uchunguzi wa vinasaba pamoja na adhabu zake.

## HITIMISHO

Sheria ya usimamizi wa vinasaba vya Binadamu ni mkombozi mkubwa dhidi ya utatuzi wa migogoro ya aina mbalimbali kijamii na kitaifa kwa ujumla yakiwemo makosa ya jinai pamoja na mashauri ya madai mahakamani. Hii ni kwa sababu majibu yake ni ya hakika kwa asilimia 99.99 na hivyo kudhihirisha kuwa ushahidi mwingi wa kitaalamu utatumika mahakamani kwa sababu ya usahihi huo, tofauti kabisa na ilivyokuwa siku zilizopita. Si hivyo tu bali sheria hii itahamasisha utafiti wa kisayansi zaidi katika kila nyanja husika ili kuleta tija ya maendeleo ya kisayansi ndani ya nchi yetu.

**Mawasiliano**:

*Katibu Mtendaji,*
*Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,*
*Mtaa wa Luthuli, Kiwanja Na. 8,*
*S.L.P. 3580,*
*DAR ES SALAAM – TANZANIA.*
*Simu: +255 22 2123533*
*Faksi: +255 22 2123534*
*Barua Pepe: lrct@irct.or.tz*
*Tovuti: www.lrct.or.tz*

© LRCT 2010

Printed By Rainbow Printers, Email: info@rainbowprinters.co.tz

*Tunahusisha yaliyopita, Tunatengeneza y a sasa na Kupanga ya baadae,*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

## *ELIMU YA SHERIA KWA UMMA*



# KUANZISHWA KWA MFUMO WA KISHERIA WA VINASABA (DNA) VYA BINADAMU NCHINI TANZANIA

## UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania ni Idara inayojitegemea iliyoanzishwa na Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania Na. 11 ya 1980, Sura 171 [Toleo la 2002]. Sheria hii inaipa Tume mamlaka ya kufanya mapitio ya sheria na kisha kufanya utafiti na kuandaa mapendekezo ambayo huwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya Mambo ya Katiba na Sheria kwa ajili ya kuchukua hatua zinazofuata. Lengo la Tume ni kuzifanya sheria za nchi ziende sanjari na mazingira ya sasa ya kiuchumi, kiutamaduni na kijamii, ili kudumisha utawala wa sheria na usimamizi wa haki nchini. Aidha, Tume inaweza kufanya utafiti na kupendekeza kutungwa kwa sheria mpya iwapo inaona kuna haja ya kufanya hivyo.

## UTAFITI WA KUANZISHA SHERIA YA KUSIMAMIA MFUMO WA VINASABA VYA BINADAMU

Mwaka 2008, Tume ilianza utafiti wa mfumo wa kisheria wa kutumia utaalamu wa vinasaba vya binadamu nchini Tanzania. Kwa kutambua umuhimu wa teknolojia ya matumizi ya vinasaba na haja ya kuwa na Sheria itakayokidhi mabadiliko ya kisayansi, Tume kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na wataalamu kutoka Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, walifanya utafiti katika baadhi ya mikoa ili kubaini madhara ya ukosefu wa sheria ya vinasaba pamoja na umuhimu wa kuwepo kwa sheria hiyo.

Baada ya kukamilisha utafiti, Tume iliandaa Ripoti yenye mapendekezo mbalimbali iliyoambatanishwa na Muswada wa Sheria na kuiwasilisha kwa Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria. Ripoti hiyo ilipelekea kutungwa kwa Sheria Inayosimamia Vipimo vya Vinasaba ya mwaka 2009.

## NINI MAANA YA VINASABA?

Vinasaba au kwa lugha ya kigeni DNA (Deoxyribonuclei Acid) ni utambulisho wa kipekee wa kila kiumbe ambao unabeba taarifa muhimu na inayorithisha tabia au umbile fulani la mhusika. Vinasaba ni kama vile kitabu cha kumbukumbu kinachohusu maisha binafsi.

Tunahusisha yaliyopita, Tunatengeneza y a sasa na Kupanga ya baadae,

Kila mtu ana vinasaba tofauti kabisa na mtu mwingine. Uchunguzi wa vinasaba hufanyika baada ya kuchukua sampuli mbalimbali kama vile; mate, nywele, mkojo, kinyesi, damu, ngozi, meno, mifupa, manii na ute wa mwanamke. Aidha, vifaa vyenye madoa au mabaki ya vitu vilivyotajwa pia vinaweza kutumika kufanya uchunguzi. Pia sampuli nyingine yaweza kutolewa toka sehemu nyingine ya mwili ili mradi iweze kutoa utambulisho wa vinasaba.

## ATHARI ZA UKOSEFU WA SHERIA INAYOSIMAMIA VIPIMO VYA VINASABA

Kabla ya sheria hii kutungwa kulikuwa na sheria nyingine za makosa ya jinai na madai ambazo ziliainisha utaratibu wa kufanya uchunguzi. Sheria hizo ni kama Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura 20 [Toleo la 2002], Sheria ya Ushahidi, Sura 6 [Toleo la 2002] na Sheria ya Uchunguzi Rasmi wa Vifo, Sura 24 [Toleo la 2002]. Hata hivyo, ushahidi uliotokana na taratibu zilizoainishwa na sheria hizi ulikuwa hauna usahihi wa asilimia 99.99 kama ilivyo kwenye taratibu zilizoainishwa kwenye sheria ya uchunguzi wa Vinasaba.

Hivyo basi, bado kulikuwa na matatizo yaliyosababishwa na ukosefu wa sheria inayosimamia vipimo vya vinasaba kama vile:-

- Watu wengi walikosa mwamko wa kwenda kupata vipimo wakihofia kuvuja kwa taarifa zao kwa sababu ya kutokuwa na sheria inayosimamia ufichuzi wa taarifa za vipimo.
- Kuwepo kwa biashara haramu ya sampuli zinazoletwa kwa ajili ya vipimo.
- Ukosefu wa stoo ya taarifa za jenetiki katika mtandao na hivyo kuleta shida kubwa katika utambuzi wa majeruhi pale panapotokea ajali mbaya kama vile ajali ya MV Bukoba na majanga ya moto.

Tunahusisha yaliyopita, Tunatengeneza y a sasa na Kupanga ya baadae,

## MATUMIZI YA VIPIMO VYA VINASABA NI YAPI?

Ugunduzi wa teknolojia ya vinasaba ni moja ya mabadiliko yaliyoleta mapinduzi na manufaa makubwa kijamii na Kitaifa kwa ujumla. Teknolojia hii ikitumika vizuri ina uhakika wa kuwa sahihi kwa asilimia 99.99.

Vipimo vya vinasaba hutumika katika maeneo mbalimbali kama vile:-

- Kuthibitisha kama wahusika wametenda makosa au la. Makosa hayo ni kama; mauaji, ubakaji na ujambazi.
- Kusaidia utambuzi wa aina mbalimbali za mimea na wanyama.
- Kutambua uasili wa binadamu na maendeleo yake tangu awali.
- Husaidia kutengeneza dawa ili kuponya magonjwa mbalimbali.
- Kutambua miili ya marehemu iliyoharibika sana.
- Hutumika katika tafiti zinazohusu magonjwa au maumbile ya kurithi katika familia moja au koo.
- Kutatua migogoro ya kesi za madai mahakamani kama vile utata dhidi ya nani ni baba wa mtoto.

## MAPENDEKEZO YA TUME

Tume ilipendekeza kutungwa kwa Sheria Inayosimamia Vipimo vya Vinasaba ikizingatia masuala yafuatayo:-

- Uchunguzi wa vinasaba ufanywe na watu wenye utaalamu wa kutosha.
- Kuwepo na stoo ya taarifa za jenetiki za watu waliohukumiwa kwa makosa makubwa ya jinai.
- Kuwepo na utaratibu madhubuti wa uchukuaji wa sampuli, ufungaji, usafirishaji wake mpaka sehemu zilipokusudiwa, nani mwenye mamlaka ya kuzipokea, utunzaji, uchambuzi na uondoaji wa sampuli hizo.
- Kwenye mashauri ya madai, kibali toka kwa mzazi au mlezi au mahakama kitatakiwa kabla